# *Shikilia Nafasi Yako Ndani Ya Kristo Yesu*

Mhubiri10:4; Kama roho yake mtawala ikiinuka kinyume chako, usiondoke mara mahali pako ulipo.kwa maana roho ya upole hutuliza machukizo yaliyo makubwa.

Shikilia nafasi yako ndani ya Kristo,maungamo yako,shikilia sana maungamo yako ndani ya Kristo (Waefeso4:15). [1]

Sasa uponyaji sio kitu ambacho unasema tu,``vema,naamini hilo.naamini hilo’’

Sasa hilo ni zuri kama ndilo uwezalo kufanya vema,kwa akili tu au unasema tu vema,…..ndio naliona hilo.Naliamini hilo’’sasa kama unalikubali kwa msingi huo,endelea kulinena tena na tena.Liseme kwa sauti lisikike. Liseme tena na tena; endelea tu kusema. Nimeponywa nimeponywa (1Petro 2:24).Liseme mpaka uwe unaliamini hasa.Na unapoliamini. Hapo sasa litaenda kufanyika.Usiwe na ushuhuda hasi kila mara unapokiri/ungama ’’vema bado najisikia vibaya leo.Nadhani ni……``unarudi nyuma kwenye mkandamizo uleule ambao ulikuwa nao mwanzoni,

Hakuna mwanaume au mwanamke hapa ambaye amebatizwa na Roho Mtakatifu na aanze kukiri kwamba.’’Naamini nimempoteza Roho Mtakatifu naamini ameondoka kwangu ninaamini…….``utaenda chini, kweli, kamwe huwezi….sikiliza kwa karibu huwezi kamwe kuishi juu ya ushuhuda wako. Yesu Kristo ni kuhani mkuu wa maungamo yetu.(Hiyo ni kweli. Sasa. waebrania 3:1,14-16.Msomi yeyote anajua kuwa neno hili``kukiri’’ ni ``kuungama’’pia inatafsiriwa sawa) Sasa akiwa mkono wa kuume wa Baba kufanya upatanisho juu ya nini? Maungamo yetu hayawezi yakatufanyia kitu mpaka kwanza umeungama/Umekiri kwamba amekifanya hicho.Unaona? wakati ulipokubali…sasa…si kuokolewa….Sikuokolewa usiku wa leo, nina furaha na kupiga makelele.Hilo silo hilo sikuokolewa kwa sababu kipawa cha Mungu kinafanya kazi ndani yangu.Nimeokolewa kwa sababu nimetimiza masharti yote ambayo Yesu Kristo aliyahitaji

kwangu.Nimeokolewa kulingana na Biblia.Unaona? Hiyo ni sawa?

Unaona. siyo kwa sababu najisikia kama nimeokoka.Shetani anaweza akakupiga kwenye kisiki kwa kujihisi kwako.

Lakini hawezi kama ni HII ASEMA BWANA.unaona?hawezi kufanya hilo. Hawezi kulivuka hilo;hilo litamshinda yeye.

Sasa wakati unapoamini kwamba umeokolewa,ukiwa umekaa katika kiti chako,popote ulipo kuwa,ulilikubali hilo nakuanza kulikiri na kuwaambia watu kuwa umeokoka.Vema,uliendelea kusema ``nimeokoka.’’(Marko16:16).Watu wakasema,``hakuna tofauti ndani yako.’’Lakini uliamini kuwa ilikuwapo. Ni sawa hiyo?Na uliendelea na kulalama kwako na baada ya muda ikatenda matendo ya haki.Majirani zako wote na kila mmoja wanajua sasa umeokolewa. Kwa sababu uliliamini ukaliungama, kwanini?kumetokea nini? Ni kitu gani kimekubadilisha?Yeye ni kuhani mkuu wa maungamo yako akiwa amekaa katika mkono wa kuume wa Baba,akilifanya kuwa zuri lile unalo liungama.(Rumi 8:33-34).Sasa ni jambo hilo hilo hata kwa ajili ya uponyaji,unampokea kama mponyaji wako,unakanusha unavyojisikia siyo kwa kujisikia; ni kwa imani (Efeso2:8-9). Sema umeponywa;amini umeponywa. Tenda kama aliyeponywa; shirikiana na wale wanao amini uponyaji;na Mungu atakuleta hasa katika ukamilifu wa afya nzuri.Hilo halishindwi. [2]

Na kama Ameliahidi anapaswa kulifanya.Kwa sababu Anapaswa kushika Neno lake.Na amekuahidi wewe jambo hilo hilo,hilo ni: kama unaweza kuamini kwamba litafanyika…``kama huwezi kuliamini;haliwezi kutokea (Yakobo1:6-7). Sasa siwezi kukufanya wewe uamini;pia huwezi kujifanya mwenyewe uamini. Inabidi Mungu akupe hilo.Ni kipawa cha Mungu kuamini,siyo imani yako,ni imani ya Mungu (Galatia2:19-20).Imani yako ya kiakili yaweza kuamini hilo sawa lakini isipokuwa imani ya Mungu ipo ndani moyoni mwako…unaona.Imani yako ya kiakili inaweza kulikubali hilo;kufanya hivyo.na hata uendelee kuamini kwa moyo wako wote mpaka Mungu alifunue kwako. Unaona?uendelee kuliamini mpaka Mungu alifunue hilo (Matayo11:25):Lakini mpaka alifunue hilo……[3]

Kuzaliwa upya ni Kristo,ni Ufunuo. Mungu amekufunulia wewe siri hii kuu.Na hilo ni kuzaliwa upya’’sasa uta fanyaje ukilipata hilo kundi lote pamoja.Ambapo ufunuo unakubaliana kikamilifu,na Mungu

akiudhihirisha kupitia Neno lake kwa matendo yale yale aliyoyatenda, akilifanya Neno lidhihirike? Oh, kama kanisa lingejua nafasi yake tu.Na siku moja litajua. Hapo,unyakuo utafanyika litakapo jitambua lilivyo [4]

Sasa,``angalia. Sasa.Na Alituambia sisi,’’kama mkikaa ndani yangu,na maneno yangu ndani yenu,mnaweza kuomba mnalotaka litafanyika’’(Yohana15:7).Sasa utambue nafasi yako katika maandiko kama mwaminio.Unaona? inabidi utambue nafasi yako kama vile Yeye alivyo tambua nafasi yake ( Luka24:25-27,44,) [5]

Katika siku arobaini za kujaribiwa na Neno la Mungu Yeye (Bwana wetu Yesu Kristo) alishinda.Nataka niwakazie jambo fulani hapa kwa dakika chache.Shetani alifanya mashambulizi makuu matatu juu yake .katika yale majaribu. Angalia,siku zote ni katika mambo matatu usisahau hayo.Alifanya mashambulizi makuu matatu kutoka kwa lililo juu hadi lililo chini alijaribu kwa uwezo wake kumshinda Yeye lakini Yeye alikuwa ni Neno.Amen.Alitumia nini? Yeye Mwenyewe, NENO. mashambulizi makuu matatu ya shetani aliyo mshambulia Yeye, lakini aliyakabili kwa Neno. kila shambulio, alilichukuwa Neno (Angalia hili sasa) kutoka lililo juu mpaka lililo chini (Mathayo 4:1-11)

La kwanza alifanya mashambulizi yake juu ya kutumia nguvu zake kuu, ambalo alilijua kuwa Yeye ni Neno; alijua nafasi Yake.Unaamini alijua? Mimi ni mwana wa Adamu’’(Matayo16:13) aliijua nafasi Yake.Na shetani akaja na kumtaka Yeye atumie nguvu zake mwenyewe juu Yake mwenyewe kujilisha. alitaka ajilishe mwenyewe Alikuwa na njaa. Mtu anapokuwa na njaa anaweza akafanya karibu kila kitu, ataiba, atanyang`anya, ataomba, ataazima. Chochote unaona? Ana hiyo shauku.Na shetani alitumia shambulizi lake kuu la kwanza juu Yake achukue nguvu zake ambazo amepewa kushindia nazo na azitumie kwa ajili Yake mwenyewe.Hakuzitumia kwa ajili Yake mwenyewe hapana.Alizitumia kwa ajili ya wengine hiyo ni kweli. Alizitumia kwa ajili ya wengine.Hiyo ni kweli Alizitumia kwa ajili ya wengine.Sio Yeye mwenyewe,hazikuwa kwa ajili Yake ingawa angeweza kufanya hivyo.Lakini uelewe vile shetani anavyotaka? Shetani anataka umjali/umsikilize.Yeye alijali tu kile ambacho Baba alisema, afanye. Hiyo ni kweli. Lakini shetani alisema``Imeandikwa, atawatuma malaika ili---‘’alisema. ndiyo, lakini

pia imeandikwa.``unaona,upo hapo. Alijua Yeye ni nani. Shetani

alijua…..lile wazo linaenda ndani kuliko yalivyoandikwa. Unaona, ni uvuvio. Kile kiini kiko ndani ya hilo. Lakini kamwe hakusikiliza ushauri wa shetani. Sasa hapa pana kitu kizuri. Unaona? Wakati mwingine shetani anaweza kukuchukua wewe na wakati unafikiri unafanya mapenzi ya Mungu. Na anaweza akakupa wewe mashauri.Nawe utayafuata.Ndio Bwana hakika yeye anaweza. [6]

Mkristo halisi anapigania nafasi yake.inabidi asimame pekee.Yeye na Mungu. Na anapigania kila inchi ya ardhi.Kwa hiyo huhitaji kumbembeleza kama mtoto (Joshua1:3). [7]

Vyovyote ilivyo,hivyo ndivyo tutakavyo.Na ninaamini ni Daudi alisema,``ningependa kuwa bawabu katika nyumba ya Bwana, kuliko kukaa katika hema za waovu (Zaburi 84:11).Unaona? haijalishi ni nini,``kuchukua nafasi yangu’’wakati mwingine inabidi utengane na kila kitu ukipendacho duniani ili uchukue nafasi yako. Mungu aliyokuitia.Nina uhakika unaweza kusoma kati kati ya mistari, kile ninacho kisema, unaona? Wakati mwingine yule mtu umpendaye sana.duniani.Inabidi mpeane mikono nao, ili uweze kuchukua nafasi yako Mungu aliyo kuitia unaona? Lakini Mungu anafanya nini? Anakugeuza wewe kutoka kile ulichokuwa. Pengine ni binti au ni mwana au chochote ulicho, kutoka pengine kwenye familia nzuri.Anakuweka mahali pengine. Kwa sababu ndiyo njia pekee ya kufanya hilo, kwa kufanya upya nia yako kwa kutii Neno la Mungu (Warumi12:2). Bila kujali ina gharama kiasi gani.Unaona haya mambo hayaji…haya kuita… [8]

Ni makusudi matatu: Moja, kujifunua mwenyewe kikamilifu; Mungu ndani ya Kristo. Pili, achukue nafasi ya kwanza ndani ya kanisa. (Ambalo ni mwili wake, Bibi arusi).Ambaye atachukua nafasi ya kwanza kupitia wao. Hilo ni sawa. Na Tatu, kuurudisha ufalme katika hali yake sahihi ambayo ulianguka, kwa sababu ya dhambi kwa Adamu wa kwanza. Kurudi kule alipotembea katika ubaridi wa jioni pamoja na watu wake, akizungumza nao, akiwa na ushirika nao,na sasa dhambi na kifo viliwatenganisha wao kutoka uweponi pake na kujifunua kwake kote.Unasoma hilo? Kabla ya misingi ya ulimwengu kuelekeza tabia zake zote,vile alivyo…..

Na sasa, yule Kristo anafanywa atambuliwe katika kanisa.Jambo lote ni ufunuo wa Mungu kumweka Hawa kwenye nafasi yake sahihi kule nyuma na mumewe. (Angalia),na Mungu ni mume wa kanisa,na kanisa ni Bibi Arusi wake. [9]

Yule Bibi Arusi ni sehemu ya mwanaume. Na mahali pekee uwezapo kulitambua hilo,ni kutambua wewe ni sehemu gani ya huyo mwanaume,lile Neno,ulicho,au huwezi kujitambua kuwa Bibi Arusi. Ni wangapi wanaliona hilo? unaona? unaona? Lazima utambue nafasi yako.Huwezi kutambua nafasi ya mtu mwingine.

Yuko Bibi Arusi mmoja. Sio madhehebu dazeni moja, lakini Bibi Arusi mmoja, hao ni wale waliochaguliwa duniani,waliokusudiwa kimbele. Kwa ajili ya hilo.Wale wanao weza kutambua nafasi yao katika Ufalme. [10]

Tuko kwenye matarajio makuu ya kumwagiwa ile nguvu ya Mungu ya kuhuisha itakayo tuleta sisi katika kujitambua nafasi zetu na sehemu na wajibu wetu wa kuwa sisi ni watu walioitwa tukiwa tumetengwa kutoka dunia,na kuwekwa wakfu kwa Mungu [11]

Kanisa halijatambua siku yake, kwa Israeli kuwa katika nchi yao ya ahadi.Hawajui wamerudi vipi pale wamewekwa pale bila fikra za mtu (automatiki) kwa nini? Nguvu za kitaifa ziliwaweka mahali pao.Sasa,nitaenda kusema kitu fulani.Nguvu za kitaifa ziliwaweka Israeli katika nchi yao.Nguvu za kitaifa zitaliingiza kanisa. Katika baraza la makanisa duniani.Lakini nguvu za Mungu zitawaweka watu ndani ya Bibi Arusi. Dunia inavuta upande huu na dunia inavuta upande huu, lakini Mungu anavuta juu , yule Roho wa Mungu,ambaye ni Neno la Mungu. (Maneno yangu ni Roho na Uzima (Yohana 6:63) litamuweka Bibi Arusi mahali pake, kwa sababu atatambua mahali pake,katika Neno;hapo sasa utakuwa ndani ya Kristo) litamuweka yeye mahali pake.

Hakuna nguvu za kitaifa zitakazo fanya hivyo lakini nguvu za kitaifa zililazimisha kuwaendesha wa Israeli kurudi kwenye nchi yao.Nguvu za kitaifa za baraza la makanisa litaendesha kila dhehebu kuingia huko lakini nguvu za Mungu zitamwinua Bibi Arusi kwenda utukufuni (Warumi 8:11) kutoka katika hilo

Oh, watu, tambueni siku yenu. Kama Yesu alivyo ona ishara ya Sodoma,na hali ya kanisa ya siku ya leo (Luka 17:26-36) [12]

Uzia, jinsi alivyokuwa mtu mkuu, ni mfano mbele ya Isaya (2Nyakati 26:1-21).Lakini alipojiinua, naye akajaribu kuchukua nafasi ya kuhani, mhuduma.Na kwa kufanya hivyo, Mungu alimpiga na

ukoma na ilikuwa ni somo kubwa kwa Isaya kujua kwamba asimtumainie mtu yeyote ila Mungu. (Isaya 6:1-8).Baadaye alikuwa hekaluni na akapaona mahali.Na hicho ndicho nilicho waambia wale wafanya biashara.Niliwaomba ndugu zangu,usijaribu kuchukua mahali popote zaidi ya kufanya biashara, chochote kile Mungu alicho kuitia ukifanye.Usijaribu kuwa mhubiri au kuchukua mahali pa mhubiri.Kwa sababu tuna wakati mgumu wa kutosha kuyaweka katika hali ya kunyooka hata hivyo,na unayaacha yamechanganyika.Kwa hiyo na tuwe kile Mungu alichotuitia tuwe. [13]

Wewe kaa kwa usahihi mahali ulipo. Unaona? Fanya kazi yako. Kile Mungu alichokuambia. Kama wewe ni kidole huwezi kuwa sikio,huwezi ukawa pua. Pua au jicho unaona? Kaa mahali pako.[14]

Na ninafikiri kwa washirika; ni kitu kizuri kwa sisi kubakia….Usijaribu kumwigiza mtu mwingine.unaona? Kuwa kile ulicho.Sisi sote tungependa kuwa Billy Graham, tuwe Oral Robert, sisi wote tungependa kuwa hivyo. Lakini kumbuka, katika ufalme wa Mungu na uchumi wake ule mkuu, kama ningekuwa (kizulia) bawabu, kama hapo ndipo mahali petu, tutakuwa tu kama wale walivyo unaona? Lakini inabidi udumu katika nafasi yako ambapo Kristo amekuweka wewe. [15]

Je uliwahi kuwazia kwa nini mtu afanye makosa? Ni kwa sababu anajaribu kutosheleza kiu ambayo Mungu ameiweka katika moyo wake ili amuonee Mungu shauku.(Yohana 7:37-39). Na hapo sasa unajaribu kuitosheleza kwa mambo ya ulimwengu.Na kamwe haitatoshelezwa mpaka itulizwe na Mungu mwenyewe, mpaka aje ndani na atulize ile shauku. Kuona kiu iliyo ndani ya moyo wa mwanadamu ( Zaburi 42:1-3 ). Kuna sehemu iliyo ya zaidi, ya mtu ambayo haitajaa.Hakuna chochote kiwezacho kuchukuwa mahali pake mpaka Mungu achukue mahali pake sahihi katika moyo wa mwanadamu [16]

Daudi mfalme aliyepakwa mafuta, watu wote wanapiga kelele na kulia kwa sauti likuwa ni sahihi, lakini alikuwa hajamuuliza nabii wa Mungu (1Nya.13).Na mtu akafa, na jambo lote likachafuliwa. Usijaribu kumfanyia Mungu upendeleo. subiri mpaka uwe katika mapenzi ya Mungu. Liache lije kwa namna yake ya kiutendaji wa hilo.``Nitaanza jambo hili kuu; nitafanya hivi,``kuwa muangalifu ndugu [17]

Na uangalie lile sanduku la Agano katika Biblia siku zote ni mfano wa Neno kwetu,kwa sababu ilikuwa ni Neno la Mungu katika lile sanduku la Agano angalia lile sanduku la Agano walivyo libeba**.**Tazama vile walivyofanya.Halikuwekwa mahali pake pa mwanzoni Mungu alivyoelekeza. Sasa, Mungu alisema pale nyuma katika sheria kwamba kama ingebidi….Namna ya kulifanya hilo.Jinsi linavyopaswa kubebwa na namna ya kulibeba.Lakini Daudi katika, upako wake—ndugu zangu, usilikose hili na dada zangu msilikose hili,haijalishi upako wako uko wa kiasi gani,lazima uje katika mahali ambapo ni njia ya Mungu. Upako wa nabii ulikuwa sawa tu, lakini alipolifanya alisisimuliwa na kutoka katika mipaka. Alifanya nini?Aliruka mstari wa mipaka aliyowekewa.

Badala ya kuliweka sanduku la agano mahali pake pa asili, alilichukuwa katika gari jipya na siyo katika mioyo ya Walawi, lilipaswa kuchukuliwa katika mabega ya Walawi ambayo yalikuwa juu ya moyo (Hesabu 4:1-6).Neno haliko akilini;liko moyoni,na siyo katika gari jipya.Hilo lilikuwa ni kitu gani? Liliwakilisha kitu fulani kipya Daudi alichokifanya pale;lilizungumzia madhehebu yoyote ambayo yangeweza kuja kutokea. Neno la Mungu halipaswi libebwe na wakuu wa serikali au maaskofu.na kadhalika,wamadhehebu.Ni ubatizo wa Roho Mtakatifu katika mioyo ya wanadamu na sio katika mfumo fulani. Roho Mtakatifu ni hazina ya upendo wa Mungu katika mioyo ya wanaume na wanawake watiifu (Rumi5:3:3-*5). [18]*

Hiyo ndiyo njia, ishi hivyo,ili kama Mungu angetaka akutumie wewe,anajua mahali sahihi pa kuja akupate wewe utakuwa uko kwenye nafasi,ukiishi maisha yaliyo safi mbele za Mungu;maneno yake ni kweli.Maisha yake ni ya kweli hapo ndipo mahali malaika wanakuja. Mwangalie Elizabeth na zakaria,watu wenye haki,wachaji wakitembea katika sheria yote ya Bwana (Luka1:5-25,57-79).Hiyo ndio namna tupaswayo kuishi, kwa hiyo Mungu anapokuwa tayari kututumia sisi, anasema``Hawa ni watu wangu.Naweza kufanya na hili kanisa chochote nitakachokifanya.wananiamini mimi.Wanasimama katika Neno langu’’unaona.hiyo ndiyo namna unayopaswa kufanya; Ishi maisha. [19]

Liangalie kanisa vile lilivyo kuja, vile linavyo endelea.Lichukue hilo tu katika akili yako mwenyewe, ninyi wana historia, ambao mnajifunza historia.Liangalieni kanisa la kiluteri-chini ya kuhesabiwa haki kwa imani.Wakiwa wanatoka tu katika ukatoliki; angalia walivyokuwa wanaenda.Halafu mwangalie Wesley akiwa anakuja

karibu zaidi, katika utakaso akilifunga katika maandiko. Angalia kwa usahihi hilo hapo katikati, yule Wesley.Halafu kilichofuata ukaja ule wakati wa pentecoste,na wakati ule wa Pentecoste na kurudishiwa karama, karama za rohoni.Sasa, angalia ule wakati unaokuja kusogea kwenye jiwe la kifuniko.Unaona ninacho maanisha? Kule kuja kwa Bwana, kunatambulishwa..Mungu na viumbe vyote vinasubiri kanisa ili liweze kupaona na kukaa mahali pake. [20]

Lakini, unaona, ni kama vile kanisa inabidi lipitie lile holi la wakosoaji. Tunapita hapo. Utaenda kuitwa``Mtakatifu anayejivingirisha’’utaenda kuitwa vitu vyote viwavyo.

Lakini kama unaweza tu kushikilia nafasi yako ndani ya Yesu Kristo, baadaye siku moja atatuchukuwa kwenye hali ya heshima (sifa).

Lakini kwanza lazima tustahimili shutuma. Hapo ndipo udogo wetu unaposimamia;hapo ndipo inapojionyesha.Yule asiyeweza kustahimili marudi ni mwana wa haramu.Na siyo mtoto wa Mungu (Waebrania 12:4-11).Haijalishi amejiunga na makanisa mangapi au amefanya nini.Bado kama hawezi kustahimili amrudi, yeye ni mwana haramu na siyo mwana halisi wa Mungu.Lakini mwana halisi wa Mungu hajali dunia inasema nini; kitu kingine chochote siyo msingi.Ameiweka akili yake kwa Kristo.Na hilo linatuliza kila kitu.ndiyo. Chochote Kristo asemacho fanya, atakifanya, kokote mwana kondoo aendako, wako pamoja Naye, na halafu unaona kule kuonekana kwake.Uwepo Wake, na vile anavyo vifanya. Yeye siku zote yuko na watu wake.Bibi Arusi Wake. Yeye anafanya urafiki naye (bibi arusi).Siku moja tutakuwepo na karamu ya arusi. [21]

Fikiria hii, Mungu siku ya pentecoste; ile Nguzo ya moto ilijigawanya, na nguzo ya moto zilikaa juu ya kila mmoja, Mungu alijigawanya mwenyewe ndani----akijigawanya mwenyewe ndani ya watu wake(Matendo2:1-4) na tumefufuka pamoja na Kristo na tumeketi mahali pa kimbinguni (ulimwengu wa Roho)(Efeso2:4-7). Tukiangalia nyuma mahali tulipotokea**.** Inatosha kwamba tunaweza kufikiria hivyo.Na inatuondolea presha, inaondolea mbali presha wakati tunapotambua nafasi tunazoshikilia. Sasa tu ndani ya Kristo kwa kule kupokea Roho Mtakatifu-uhai wa Mungu mwenyewe (lile neno la kigiriki``Zero’’ambalo lina maanisha uhai wa Mungu mwenyewe) ukikaa ndani yako (Yohana 5:24) na huwezi kufa kamwe,

kama Mungu asivyo weza kufa. (Amen). Tukiusubiri wakati ule wa ukombozi wa mwili.(Warumi 8:22-23). Na sasa tayari tumekwisha kufa na uhai wetu umefichwa ndani ya Mungu kwa njia ya Kristo na kutiwa muhuri na Roho Mtakatifu.Shetani hayuko tena kwenye picha. Na tunapokaa mahali pamoja kama hivi katika mahali pa kimbinguni (ulimwengu wa Roho) pamoja na Kristo, ndani yake hapo sasa tunaweza kupunguza (presha) nguvu ya mkandamizo [22]

Mahali pa kimbinguni ni nini? ni nafasi ya mwaminio ndani ya Kristo ambapo mwaminio anasimama ndani ya Kristo,katika (ulimwengu wa kiroho) mahali pa kimbinguni. [23]

Ili mradi uko ndani ya Kristo, uko katika Biblia;uko ndani Yake katika Biblia.Unaona?Ili mradi uko ndani ya Kristo, basi uko katika ukamilifu wa biblia.unaona? Uko katika nafasi yako kamili unapokuwa ndani ya Kristo.Wote mnaelewa hilo? [24]

Mafundisho ya Biblia kwa kawaida yanaogopesha kidogo, unaona,ni kama kutembea katika barafu nyembamba,tunavyoita,lakini tunajisikia pengine kwamba mahali hapa na kwa wakati huu, ninaona ni vizuri kulileta kanisa kwa kile nifikiriacho,kwenye ufahamu wote,mahali petu tulivyo ndani ya Kristo Yesu.Na wakati mwingine nafikiri kuhubiri ni kitu cha ajabu sana,lakini naamini wakati mwingine mafundisho huvuka hapo,na ni muhimu kwa kanisa.

Sasa mahubiri, mara nyingi yanamnasa mdhambi,yanamleta yeye chini ya hukumu kwa Neno.Lakini mafundisho yanamrudisha mtu mahali pake vilevile alivyo na hatuwezi kuwa na imani kwa usahihi mpaka tumejitambua sisi hasa ni nani. [*25*]

Nukuu za kingereza
[1] Kung’ang`ania 63-1116E aya 199b
[2] Kazi zinanishuhudia 53-0216 ayaE-9-E-11
[3] Matendo ni imani iliyodhihirishwa 65-1126 aya326b-327
[4] Kristo ni siri ya Mungu 63-0728.aya37-4
[5] Imani kamilifu 63-0825E.aya94
[6] Nitawezaje kushinda 63-0825M.aya114-119
[7] Kung`ang`ania 64-0305.aya94
[8] Nguvu ya kubadilishwa. 65-1031M.aya76-77
[9] Kristo ni siri 63-0728,aya 24-5,25-1,36-1
[10] Makao ya baadaye 64-0802 aya 38-1b,57-3
[11] Je Mungu hubadili nia yake 65-0418E aya 1
[12]Kutambua siku yako 64-726M-aya192-193
[13] Kuwekeza 63-0126.aya E-15a

---

*jiwe la kiroho la kujengea na. 170 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69 D – 75328 Schomberg, Germany (+49) 72357613 Fax : (+49) 72353306. www.biblebelievers.de*

---

*Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia.*

*(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)*

*Kwa nakala zaidi za kiingereza, Kiswahili andika kwa*
*Charles E. Kanju*
*Box 553 Korogwe Tanga*
*Email: chaelika@live.com*
*Cell phone: 0784 704299/ 0718230098*